

MAANA NA MAELEZO KUHUSU UCHAGUZI MKUU

Uchaguzi ni njia ya msingi iliyokubalika ambayo jamii huitumia kupata viongozi Kidemokrasia. Sifa mojawapo ya Uchaguzi wa Kidemokrasia uliohuru na wa haki ni Uchaguzi kufanyika kwa Siri ambapo jamii hupiga Kura kwa viongozi wanao wahitaji na wanaowaona wanafaa kwa ajili ya kuwaongoza na maendeleo ya jamii husika.

Uchaguzi wa Kidemokrasia hufanyika mara kwa mara katika vipindi vinavyoeleweka, Uchaguzi kutoa fursa sawa kwa wagombea wote katika ngazi husika kuruhusu waangalizi wandani na nje kufuatilia mchakato mzima wa Uchaguzi.

Uchaguzi Mkuu ni mchakato mzima wa wananchi au jamii kupiga Kura kuchagua wawakilishi wao kuanzia ngazi ya kata kwa maana ya Madiwani, Jimbo kwa maana ya Wabunge na Uchaguzi wa Rais wa nchi.

Tanzania inatumia Mfumo wa Uchaguzi ambao Mgombea anayepata Kura nyingi halali kuliko Mgombea mwingine yeyote ndiye hutangazwa kuwa mshindi (*First - Past - the Post*). Hii, ni Kwa mujibu wa Ibara ya 41(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977, kifungu cha 35 F (8) na 81(a) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 82(a) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

Mfumo mwingine unaotumika ni ule wa Uwiano wa Kura (*Proportional Representation*) ambao hutumika kupata Wabunge Wanawake wa Viti Maalum kama ilivyofafanuliwa katika Ibara ya 78 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mfumo huu pia hutumika kuwapata Madiwani Wanawake wa Viti Maalum kwa uwiano wa Viti vya Udiwani vya Kata ambavyo kila Chama kimeshinda katika Halmashauri husika. Hii, ni kwa mujibu wa Kifungu cha 35 (1) (d) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 na Kifungu cha 24(1) (c) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288.